

## Kukomesha Mtiririko: Ujumbe muhimu

*Kukomesha Mtiririko: Jinsi dunia inavyoweza kukomesha uchafuzi wa plastiki na kukuza uchumi unaotumia bidhaa tena na tena*, ni ripoti inayozingatia masuluuhisho, inayotoa mienendo thabiti, mabadiliko ya masoko na ya sera. Inachapishwa tunapoelekea [awamu ya pili ya mazungumzo](#) kuhusu chombo cha kisheria kitakachotumiwa kukomesha uchafuzi wa plastiki. Inalenga kuimarisha maarifa kuhusu kiwango na hali ya mabadiliko yanayohitajika katika uchumi wa plastiki ili kufikia lengo hili.

### Ripoti hii inatoa “dira” kwa serikali na mkakati kazi kwa mashirika ya biashara kukomesha uchafuzi wa plastiki kufikia mwaka wa 2040:

- Kupunguza uchafuzi wa plastiki kwa asilimia 80.
- Kupunguza uzalishaji wa plastiki inayotumika mara moja kwa nusu.
- Uwezo wa kuokoa pesa na gharama zinginezo kwa jumla za dola za Marekani trilioni 4.5 kufikia mwaka wa 2040.
- Kubuni nafasi za kazi 700,000, haswa katika nchi za kipato cha chini.
- Dira hii inategemea tu teknologia na masuluuhisho yaliopo tayari ila yanahitaji kushughulikiwa kwa wakati mmoja kwa dharura na sekta zote. Kusita kwa kipindi cha miaka mitano kutekeleza mabadiliko yanayohitajika kunamaanisha gharama za ziada za tani milioni 80 milioni za uchafuzi wa plastiki kufikia mwaka wa 2040.
- Mbinu inayojumuisha sheria na sera ni chombo muhimu cha kushughulikia masuluuhisho katika mfumo mzima ni muhimu kwa sababu huimarishana kuwezesha kufikia lengo la kufanya mabadiliko uchumi.
  - Kupunguza kiwango cha changamoto kwa kukomesha matumizi ya plastiki isiyohitajika inayosababisha matatizo.
  - Mabadiliko matatu katika masoko – kutumia tena, kuchakata, matumizi mapya na matumizi mbalimbali .
  - Kukabiliana na utamaduni kuwa plastiki haiwezi komeshwa, kutumiwa tena, kuchakatwa na kuwa na mbadala.
- Kwa kila mabadiliko yanayohitajika (kutumia tena, kuchakata, matumizi mapya na matumizi mbalimbali), ripoti hii inaangazia kuhusu yale yanayoweza kutokea kwa wazalishaji wa polima na kemikali, wabadalishaji wa plastiki, watengenezaji bidhaa/chapa, wauzaji wa bidhaa, serikali, watumiaji wa bidhaa, kampuni zinazoshughulikia taka na kampuni za uchakataji.

### Kutumia tena:

- Kuachana na plastiki isiyohitajika inayosababisha madhara, pamoja na kuitumia tena na matumizi mapya, ni mbinu mwafaka, kwa sababu inapunguza taka chanzoni.
- Kutumia tena inajumuisha chupa zinazoweza kujazwa tena, mifuko inayoweza kutumika tena, vitu vikuu vya kujazia kwenye maduka makubwa na ya rejareja, mipango ya kurejeshewa pesa unaporudisha, mipango ya kurejesha mifuko ya kupakia, kuosha na kukarabati, vyombo na mifuko ya chakula, huduma za usajili wa upakiaji kwa ghamama ya chini na vifurushi dhabit vya bidhaa.
- Kuimarishe soko la bidhaa zinazoweza kutumika tena na kujazwa badala ya uchumi wa kutupa bidhaa kunamaanisha kuhakikisha kuwa soko la utumiaji tena ni imara kibashara kuliko la plastiki inayotumika mara moja.
- Haya ni mabadiliko makuu zaidi ya soko, yanayoweza kupunguza asilimia 30 ya uchafuzi wa plastiki kufikia mwaka wa 2040.
- Kutumia tena na mifumo mipy ya matumizi ni mipango nafuu zaidi, inayokadiriwa kupelekeea kuokoa dola za Marekani 1,289 kwa kila tani ya plastiki inayotumika tena na dola za Marekani 516 kwa kila tani ya plastiki kwa mifumo mipy ya kushughulikia plastiki.
- Masuluhihi ya kutumia tena plastiki isiyodumu yapo kiteknolojia, ijapokuwa uwekezaji unahitaji ili kuunga mkono mabadiliko kuelekeea uchumi unaodumisha bidhaa kwa thamani ya juu zaidi iwezekanavyo.
- Malengo yaliyowekwa kwenye sheria (kama vile Sheria ya Ufaransa ya Kupambana na Taka, 2021), maeneo ya kukusanya, kutuza wanaorejesha, utaratibu wa kukabiliana na taka (ikiwa ni pamoja na kuosha na usafi), kuweka lebo na mawasiliano, kunaweza kuhakikishia soko wakati wa kuzingatia uwekezaji katika bidhaa na mbinu zinazoweza kutumika tena.
- Sera sawia na hizi zinapaswa kuchukuliwa katika nchi zote ili kunufaisha uchumi na kurahisisha mashirika ya biashara kufanya mabadiliko kutoka kwa utupaji hadi uchumi unaotumia bidhaa tena na tena.

### **Kuchakata**

- Kuhakikisha kuwa uchakataji unakuwa mradi thabiti na wenye manufaa zaidi kunaweza kupunguza kiwango cha uchafuzi wa plastiki kwa asilimia 20 ya ziada na kuongeza kiwango cha plastiki inayoweza kutumika tena kwa uchumi kutoka asilimia 21 hadi 50 kufikia mwaka wa 2040.
- Kuweka sheria kunaweza kupelekeea kuondolewa kwa utiaji wa rangi, pigimenti na viongezaji vyote vinavyoathiri sayansi ya kuchakata; ikijumuisha vitu vilevile kwa aina na muundo wa plastiki; kuondoa na/au kupiga marufuku polima ambazo ni vigumu kuchakata na zenye matatizo; kuongeza bidhaa zinazoweza kuchakatwa na watumizi kwenye vitu mpya; kuondoa kemikali hatari; kuweka viwango na kuimarishe lebo ili kuboresha utenganishaji wa taka.
- Uondoaji wa ruzuku kwa mafuta ya visukuku, ambayo kwa sasa hutumika kutengeneza plastiki ambayo haijawahi kutumika kwa bei nafuu kuliko vitu vinavyochakatwa, kutasawazisha nyanja ya uchakataji.

- Ikiwa ni pamoja na nyenzo chache kabisa ya bidhaa zilizochakatwa katika ununuzi wa umma au mikataba ya muda mrefu ya uondoaji itahakikisha polima iliyochakatwa inahitajika.
- Kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa taka kutahitaji ili kukuza mabadiliko ya kuongeza kuchakataji.
- Uchakatajii kiufundi unapendelewa kwa kuzingatia gharama zake na uzalishaji wa hewa chafu. Hata hivyo, uchakataji wa kemikali unahitajika kwa takriban asilimia 5 ya kiasi cha plastiki isiyodumu kufikia mwaka wa 2040, ambayo haiwezi kuchakatwa kwa kutumia mitambo.
- Meksiko ni mfano wa nchi ambazo mazingira mwafaka yaliwezesha uwekezaji katika uchakataji, na kuimarisha kiwango kutoka asilimia 8.8 mwaka wa 2002 hadi asilimia 56 mwaka wa 2018.

### **Matumizi mapya na matumizi mbalimbali**

- Kubadilisha kwa uangalifu bidhaa kama vile mifuko ya plastiki, vikopa vya plastiki na vitu vya plastiki vya kupakia chakula na bidhaa zilizotengenezwa kutoka kwa nyenzo mbadala (makaratas, vitu vinavyoweza kuoza, plastiki iliyochakatwa, n.k.) ni fursa ya uvumbuzi na maendeleo ya kiuchumi yanayoweza kupunguza asilimia 17 ya uchafuzi wa plastiki.
- Utoaji wa njia mbadala kwa plastiki ni sharti kila mara uungwe mkono na tafiti za tathmini mzunguko mzima ili kuthibitisha iwapo njia mbadala ni bora kuliko plastiki inayoondolewa.

### **Kushughulikia utamaduni wa uchafuzi wa plastiki:**

- Ingawa kuhamia kwa wakati mmoja kwa kutumia tena, kuchakata, na matumizi mapya kunaweza kupunguza asilimia 80 ya uchafuzi wa plastiki, hatua bado zitahitajika ili kushughulikia tani milioni 100 za plastiki kutoka kwa bidhaa zisizodumu kila mwaka, kufikia mwaka wa 2040: kiwango sawa na takribani uzito sawa na makontena milioni tano ya usafirishaji wa bidhaa, ambayo - yakichunguzwa - yatasafiri kilomita 30,000 au safari ya kwenda na kurudi kutoka New York City hadi Sydney.
- Maikroplastiki, hasa kutoka kwa magurudumu, masisawa, nguo, na vipodozi, zinaweza kushughulikiwa kwa kupunguza masafa ya magari, kuunda upya magurudumu na mabadiliko ya mienendo, uboreshaji wa miundo na utengenezaji wa nguo, kuongeza vichungi kwa mashine ya kufua, kuboresha uzalishaji na masoko ya marisawa ya plastiki na kuwezesha usafiri wake salama, na kupiga marufuku matumizi ya maikroplastiki inayoongezwa kimakusudi kwa vipodozi.
- **'Ghost gear'** au zana za uvuvi zilizoachwa, kupotea na kutupwa – nyavu, mishipi, kamba na vyombo vya kuvulia samaki vilivyoachwa – vinaweza kusababisha angalau asilimia moja ya jumla ya uchafuzi wa plastiki. Masuluuhisho yanahita juhudi zilizoratibiwa ili kusitisha uchafuzi chanzioni huku yakiboresha ushughulikiaji wa taka kwenye mazingira.
- **Masuluuhisho kwa utupaji taka** yanasalia kuwa chaguo bora zaidi ikilinganishwa na uchomaji wazi wa taka: tani moja ya taka za plastiki inayojikuta kwenye mtambo

wa uteketezaji huzalisha takribani asilimia 20 ya GHG kuliko tani sawa na hiyo ikichomwa mahali wazi.

- Madampo yaliyotengenezwa na wahandisi ndiyo njia ya gharama nafuu ya kutupa taka. Hata hivyo, maikroplastiki inaweza kuingia katika mazingira, hata katika madampo safi zaidi.
- Gharama za uzalishaji wake hupotelea kwenye uchumi plastiki inapotupwa kwenye madambo. Pia huchukua nafasi kubwa, mara nyingi karibu na miji.
- Wakati utupaji wa taka katika nchi ambako taka hiyo huzalishwa hupendelewa, usafirishaji wa taka ya plastiki ambayo haijachanganywa na haina madhara kati ya nchi jirani inaruhusiwa ikiwa kuna Idhini ya Awali inayozingatiwa.
- Serikali ya kitaifa inafaa kuzingatia uwajibikiaji wa ushughulikiaji wa taka.

#### Ajira:

- Kufikia mwaka wa 2040, mabadiliko kuelelea uchumi unaotumia bidhaa tena na tena yanaweza kupelekea kazi zaidi za ziada 700 000 kuliko iwapo tutaendelea na mambo kama kawaida.
- Watu maskini katika nchi za kipato cha chini ndio watakaonufaika zaidi kutokana na kazi mpya zinazohusishwa moja kwa moja na plastiki isiyodumu: ukusanyaji, utengaji, uchakataji, ukabilianaji, uoshaji wa vitu vinavyoweza kutumika tena na kuvitumia tena, yote hayo yanahitaji zaidi kuliko utengenezaji wa plastiki mpya.
- Katika ‘mabadiliko ya haki’ kuelekea uchumi usiochafua mazingira na shirikishi, wafanyakazi wenye ujuzi wa hali ya juu katika uzalishaji wa plastiki ambayo haijawahi kutumika na katika ubadilishaji wa bidhaa za plastiki wana uwezo wa kupata kazi mbadala katika uchumi unaotumia bidhaa tena na tena/ kwengineko.

#### Ufadhilli

- Kwa ujumla, mabadiliko ya kimfumo yanayohitajika ili kuokoa dola za Marekani trilioni 1.27 kwa kuzingatia gharama za uwekezaji, uendeshaji shughuli na gharama za usimamizi na mapato ya kuchakata. Dola za Marekani trilioni 3.25 zaidi zitaokolewa kutokana na mambo ya nje yaliyoepukwa.
- Uwekezaji na ufadhilli kwa gharama za uendeshaji wa shughuli unaohitajika chini ya mabadiliko ya mifumo ni kidogo ikilinganishwa na kuendelea na mambo kama kawaida ila kutakuwa na changamoto kiasi, kama vile mtaji wa juu unaohitajika kwanza. Uingiliaji kati utahitajika, kwa mfano ili kuhakikisha kwamba mabadiliko hayo yana manufaa ya kiuchumi na kifedha kwa wahusika wote.
- Kiasi kikubwa cha uwekezaji unaohitajika unawezekana kwa kuhamishia uwekezaji uliopangiwa vifaa vipyta vya uzalishaji wa plastiki (isiyohitajiki tena kwa kupunguza nyenzo zinazohitajika) hadi kwa miundomsingi inayohitajika ya kutumia bidhaa tena na tena.
- Gharama za juu zaidi katika uchumi wa kutupa na uchumi wa kutumia bidhaa tena na tena. Mara tu sheria zitakapohakikisha kwamba plastiki zinazoundwa zinaweza kutumika tena na tena, mipango iliyosanifiwa vyema ya Uwajibikaji Mpana wa Mzalishaji wa Bidhaa (EPR) inaweza kulipia gharama kamili za kuhakikisha mfumo unaweza kutumia bidhaa tena na tena. Katika Muungano wa Ulaya (EU), ufadhilli

wa ukusanyaji, uchakataji na uwajibikaji wakati wa kutupa mifuko baada ya matumizi, taka kutoka kwa vifaa vya umeme na kielektroniki, betri, hutolewa kwa wazalishaji, na kupunguza gharama za ushughulikiaji wa taka kwa zaidi ya asilimia 50 (nchini Ufaransa) na kupelekea viwango vya zaidi ya asilimia 80 ya uchakataji wa mifiko ya kupakia (nchini Ubelgiji).

- Sera kama vile ushuru wa uzalishaji wa plastiki ambayo haijawahi kutumika zinaweza kuleta mabadiliko ya soko na kufanikisha mabadiliko yote matatu yanayohitajika.
- Matumizi ya kibali cha mauzo ya plastiki ni suluhisho la mfumo wa soko, linaloundwa kwa kuzingatia kibali cha mauzo ya gesi ya ukaa. Hata hivyo, mfumo huo hauna vigezo na hatua zinazokubaliwa kimataifa za kutunza haki za mazingira na jamii, hasa za sekta ya ukusanyaji taka zisizo rasmi.
- Katika [Kikao cha Kwanza cha Kamati ya Majadiliano ya Serikali Mbalimbali](#), Ghana ilielezea umuhimu wa kuanzisha mfuko wa urathi ambapo wasimamizi wa viwanda katika sekta ya plastiki wanaweza kuchangia kutenga rasilimali za kuondoa plastiki ambayo tayari imeingia kwenye mazingira, hasa kati nchi za kipato cha kati na cha chini.

### **Mapendelezo ya kukomesha uchafuzi wa plastiki katika ngazi ya kimataifa**

Vipengele na sera zifuatazo zinaweza kuzingatiwa na serikali wakati wa kuunda sheria za kukabiliana na uchafuzi wa plastiki na kuunda ajenda ya hatua zitakazofuata:

- Punguza ukubwa wa tatizo kwa kukubaliana kuhusu vigezo vya bidhaa za plastiki na kemikali zinazohusiana ambazo zinaweza kupigwa marufuku.
- Anzisha msingi wa maarifa ya kuvuka mipaka.
- Kuharakisha utumiaji tena kwa kuzingatia malengo na kanuni za mabadiliko ya soko na wajibu wa kimataifa, ikijumuisha sheria kuhusu viwango vya chini kabisa vya uendeshaji shughuli vinavyohitajika vya mipango ya EPR na viwango vya muundo unaoweza kutumika tena.
- Kuimarisha uchakataji kuitia muundo na viwango vya usalama vinavyohitaji bidhaa zote za plastiki kuweza kutumika tena na kuchakatwa, kuwekwa lebo, shabaha za uchakataji wa kiwango cha chini, sheria za utaratibu maalum katika sekta isiyo rasmi ya taka, na viwango vya chini vya kemikali zinazotumika na mipango ya kurejeshewa amana.
- Matumizi mapya na matumizi mbalimbali kwa kutambua plastiki ya kubadilishwa na njia mbadala zinazokubalika, pamoja na kuweka viwango vya plastiki inayoweza kuoza/kuharibika.
- Kushughulikia urithi wa plastiki, kwa kutumia viwango vya kawaida vya utupaji salama.
- Hakikisha ushiriki, taarifa, na upatikanaji wa haki kwa mashirika ya uraia, wasomi, mashirika ya watumiaji bidhaa, viwanda, sekta binafsi na watu binafsi.
- Zingatia mabadiliko ya mienendo na maamuzi binafsi, ikijumuisha masuala ya jinsia na kizazi, kama [inavyofanywa](#) na Serikali ya India.